# Kiswahili Katika Elimu ya Juu

**Wahariri**

Ernest Sangai Mohochi
Mwenda Mukuthuria
James Omari Ontieri

# Sura ya Kumi na Sita

# Hatua za Maendeleo Katika Tafiti Zilizofanywa Katika Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Cha Kenyatta

*Pamela Muhadia Ngugi*

## Ikisiri

*Mojawapo ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Ominde ya mwaka 1964 ilikuwa kuanzishwa kwa idara ya Isimu na lugha za Kiafrika katika Kitivo cha Sanaa katika Chuo Kikuu cha Nairobi mwaka 1969 ambapo somo la Kiswahili lingepewa kipaumbele. Baadaye, katika mwaka 1985, Chuo cha Kenyatta kilifanywa Chuo Kikuu cha tatu . Katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika ilianzishwa mwaka wa 1987, ambapo mafundisho katika taaluma ya fasihi na fasihi hutolew. Vilevile tafiti katika maeneo mbalimbali ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika na fasihi yake hutolewa. Idara hii huendesha programu za uzamili na uzamifu. Matokeo yake, yamedhihirika kupitia kwa tafiti mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Lengo la sura hii ni kueleza na kutathmini mwelekeo ambao tafiti hizi zimechukuwa tangu kutambuliwa kwa lugha hii kama somo katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.*

## Utangulizi

Elimu ya vyuo vikuu imekua na kupanuka kwa kasi sana tangu mwongo wa kuanzia 1990 na hivyo basi kutoa nafasi kwa wanafunzi wengi waliohitimu kuweza kujiunga na vyuo hivi. Programu mbalimbali zimezinduliwa ambazo zinawawezesha na hata kuwarahisishia wanafunzi kuweza kupata masomo kwa njia inayowafaa wenyewe. Vilevile, pamekuwa na mageuzi makubwa ambayo yametokea katika mitaala, ufundishaji na mbinu za ukadiraji wa masomo kwa lengo la kuboresha masomo ya vyuo vikuu. Kwa mfano, matumizi ya teknolojia mpya yanahimizwa na kutekelezwa katika vyuo vingi kama mbinu mbadalia ya kufunzia. Vyuo vingi vimefungua mabehewa katika miji mingine kwa lengo la kuwafikia wanafunzi wengi katika kaunti mbalimbali. Pia, vyuo vya kimataifa vimeanzisha mabewa humu nchini kwa lengo la kuleta elimu karibu na wanafunzi ambao wangependa kujiunga na vyuo hivi.

Wakati huu ambapo mabadiliko yanatokea katika mfumo mzima wa elimu ya vyuo vikuu, pana haja ya kutathmini hali ya tafiti ambazo zimefanywa kwa lengo la kubainisha maendeleo ambayo yamepatikana katika vitengo mbalimbali vya ufundishaji. Sura hii imelenga kubainisha tafiti mbalimbali zilizofanywa katika idara ya Kiswahili katika chuo cha Kenyatta kama njia ya kuonyesha maendeleo ya kiusomi katika idara hii. Utafiti huu umejadiliwa mintaarafu mambo muhimu yafuatayo: jumla ya tafiti zilizofanywa kuanzia mwaka 1991 katika maktaba ndogo ya idara ya Kiswahili; maeneo mapana na vitengo mbalimbali vilivyoshughulikiwa katika tafiti hizi. Hatimaye, sura hii itatoa maoni yanayoweza kutumiwa katika kuimarisha kitengo hiki ambacho ni mojawapo ya vitengo muhimu wa vyuo vikuu.

**Usuli wa Utafiti katika Vyuo Vikuu**

Kabla ya kuelezea hali ilivyo katika chuo cha Kenyatta, ni vizuri kuelewa falsafa ya kijumla kuhusu malengo ya kufundisha lugha ya Kiswahili. Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili ni mojawapo wa mapendekezo yaliyotolewa na tume ya Ominde ya 1964 (Republic of Kenya, 1964). Malengo ya kufunza Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu yananuia kufanikisha malengo ya elimu kwa ujumla nchini Kenya vikiwemo vyuo vikuu. Malengo haya ni:

1. Kukuza utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa
2. Kuendeleza ujenzi wa taifa kiuchumi, kiteknolojia na kijamii
3. Kujiendeleza na kujitimilisha kibinafsi
4. Kuendeleza uadilifu na amali za kidini
5. Kuhimiza usawa wa kijamii na uwajibikaji
6. Kukuza, kuhifadhi na kuthamini tamaduni za jamii mbalimbali nchini Kenya
7. Kuendeleza uhusiano wa kimataifa na kudumisha mwelekeo ufaao kwa mataifa mengine ulimwenguni
8. Kuendeleza uhifadhi wa afya bora na mazingira

Ni kutokana na malengo haya, ambapo tume hii ilipendekeza kuanzishwa kwa idara ambayo itashughulikia sio tu ufundishaji wa walimu wa Kiswahili, bali pia ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi ili kuchangia katika kuiendeleza lugha hii. Ukweli ni kwamba, Kiswahili sasa ni lugha ya kitaifa, lugha rasmi na hata lugha ya kimataifa inayoendelea kushamiri kila kuchao. Kuundwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kumechangia matumizi pamoja na masomo ya Kiswahili kote nchini. Kiswahili ni mojawapo kati ya lugha rasmi za Umoja wa Afrika. Ni kutokana na upanuzi huu ambapo, pamekuwa na tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa na zinaendelea kufanywa katika idara nyingi za Kiswahili katika vyuo mbalimbali. Kwa mujibu wa Musau na Ngugi (1997), kufikia mwaka wa 1996,

palikuwa na zaidi ya tasnifu 95 katika kiwango cha uzamili na uzamifu kutoka vyuo vya Nairobi na Kenyatta; tasnifu hizi ni zile zilizoandikwa humu nchini. Ukweli ni kwamba, tafiti kuhusu lugha ya Kiswahili zinaendelea kufanywa humu nchini na katika vyuo vingine katika sehemu mbalimbali ulimwenguni.

Malengo ya idara ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Kenya ni kuwaandaa wanafunzi ili wafuzu kuwa wataalamu wenye ujuzi unaoweza kutumiwa kote nchini, (Simala 2002). Aidha, inatarajiwa kuwa baada ya masomo yao, wanafunzi watatoa mchango wao katika kuiendeleza nchi katika nyanja mbalimbali ikizingatiwa kuwa taaluma ya Kiswahili ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi za Kiafrika, na hasa Afrika Mashariki. Ni katika misingi hii, ambapo kozi ya utafiti ni ya lazima kwa kila mwanafunzi anayejiunga na chuo kikuu katika kiwango cha uzamili. Kozi hii huwapa wanafunzi mbinu ambazo zitawashirikisha wanafunzi-watafiti katika kuchunguza, kupanga, kuchanganua na kuwasilisha matokeo katika ripoti. Kozi hii hivyo basi, inakuwa jukwaa la maandalizi ya watafiti wa baadaye katika taaluma ya Kiswahili .

Kama anavyohoji Simala (2001:12), "Utafiti unachukuliwa kuwa fursa nzuri kwa wanafunzi kuonyesha kwa vitendo yale ambayo wamejifunza katika mawanda mbalimbali ya taaluma ya Kiswahili kama vile isimu, fasihi na lugha." Hii ni njia moja ya kuwahamasisha wanafunzi ili washiriki ipasavyo katika utafiti katika Kiswahili ambao utaonyesha hali halisi ya lugha hii katika jamii.

**Tafiti Zilizofanywa katika Idara ya Kiswahili**

Tangu idara ya Kiswahili kuanzishwa katika chuo cha Kenyatta mwaka wa 1985, takribani wanafunzi 530wamesajiliwa kwenye progamu ya uzamili na uzamifu. Wanafunzi wa uzamili wanapojiunga na programu hii, wao husomeshwa kozi mbalimbali za isimu na fasihi kwa mihula mitatu. Baada ya kozi hizi, kila mwanafunzi anatarajiwa awe amejiamulia maeneo yake ya utafiti, ikiwa ni fasihi au isimu. Anatakiwa aandike makala-dhanishi ambayo inajadiliwa katika kikao cha kamati ya masomo ya uzamili kisha kamati hiyo inamteulia wasimamizi. Kwa upande mwingine, wanafunzi wa uzamifu huanza utafiti wao moja kwa moja katika eneo waliloteua kwa kuandika makala dhanishi, kuteuliwa wasimamizi na kisha kuendelea na utafiti wao.

Jumla ya tasnifu **179** ndizo zimekamilika kufikia mwaka 2015. Kati ya hizi, **165**ni za kiwango cha uzamili, nazo **14** ni za kiwango cha uzamifu. Matokeo haya yanabainisha kuwa, ingawa wanafunzi wengi hujiunga na programu ya uzamili, ni asilimia thelathini na nne (34%) tu, ambao wameweza kukamilisha masomo yao. Ina maana kuwa, wanafunzi wengi wametamauka katika kuendelea kufanya utafiti baada ya kumaliza masomo ya darasani. Katika kiwango cha uzamifu, inaonekana kuwa wanaojiunga na programu hii ni wachacahe sana. Idadi hii ndogo ya wanafunzi katika programu ya

uzamifu inatokana na sababu kuwa, kwa muda mrefu, idara haikuwa na wahadhiri wa kutosha waliohitimu kwa kiwango cha uzamifu ambao wangewasimamia wanafunzi katika tafiti zao. Tatizo lingine linatokana na gharama ya kufadhili masomo ya uzamifu kwa wanafunzi wengi ambao wangetaka kujiunga na programu ya uzamifu. Vilevile baadhi ya wanafunzi / walimu walipata ufadhali na wakajiunga na vyuo vya ngambo kwa masomo ya uzamifu. Kwa mfano, miongoni mwa wahadhiri walio na shahada za uzamifu, wahadhiri sita wamepata mafunzo kutoka vyuo vya nje. Mafunzo yao yalifadhiliwa na serikali kama vile, Ujerumani, Austria na kadhalika. Hata hivyo, ni vizuri kutaja kuwa, hivi karibuni, idadi ya wanafunzi ambao wamejisajilisha katika programu ya uzamifu imeanza kuongezeka. Wengi wao ni wahadhiri katika vyuo mbalimbali humu nchini, na wangetaka kutekeleza matakwa ya Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu (Commission for University Education- CUE) ambayo imependekeza kuwa, kufikia mwaka wa 2018, wahadhiri wote katika vyuo vikuu wawe wamepata shahada ya uzamifu.

**Vitengo Vikuu vya Mafunzo**

Vipo vitengo viwili vikuu vya mafunzo katika idara ya Kiswahili; kitengo kinachoshughulikia masuala ya fasihi na kile kinachoshughulikia isimu. Vitengo hivi vimegawika katika vitengo vingine mahsusi kama tukavyovijadili baadaye. Kufikia sasa hivi, idadi ya tafiti zilizofanywa katika kitengo cha fasihi ni 98; ilhali tafiti zilizofanywa katika kitengo cha isimu ni 67 katika kiwango cha uzamili. Katika kiwango cha uzamifu, tafiti 8 zimeshughulikia masuala ya fasihi nazo 6, zimeegemea katika uwanja wa isimu.

Kutokana na matokeao haya ya kimsingi, tunaweza kusema kuwa tafiti katika idara ya Kiswahili zimeweza kupiga hatua ingawa kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na wanafunzi waliojisajili kufikia sasa. Kwa mfano, tunaona kuwa wanafunzi waliofuzu katika miaka ya awali walikuwa wachache mno katika kiwango cha uzamili. Pili tunaona kuwa wanafunzi wengi hawakamilishi masomo yao. Hali hii inahaitaji kuchunguzwa na wadau katika idara na hata katika chuo kwa jumla. Tunaweza kuchukulia kuwa, hapo zamani, wanafunzi wengi katika daraja ya kwanza hawakuwa na motisha ya kujiunga na masomo ya uzamili , hivyo basi kuchangia katika usajili mdogo wa wanafunzi katika idara ya Kiswahili. Vilevle, palikuwa na masharti yaliyowazuia wanafunzi kujiunga na masomo ya uzamili. Kwa mfano, vyuo vikuu havikuruhusu wanafunzi waliokuwa wamefuzu kwa kiwango cha *Second Class Honours, Lower Division* kujiunga na progaramu ya uzamili isipokuwa wale waliopata *Second Class Honours, Upper Division.* Maendeleo makubwa yanajitokeza kuanzia mwaka wa 2005 na kwenda mbele ambapo idadi ya wanafunzi wanaaojisalisha katika programu ya uzamili inaanza kuongezeka. Ongezeko hili linatokana pia na kuongezeka kwa vyuo vikuu nchini Kenya vikiwemo vya Kiserikali na kibinafsi.

Vilevile, ongezeko hili linatokana na Tume ya Kuajiri walimu kuanzisha mpango wa kuwaruhusu walimu kuendeleza taaluma zao kwa kupata mafunzo zaidi hasa katika masomo wanayofundisha. Hata hivyo, tunaona kuwa idadi ya wanaojisajili na wanao kamilisha haziambatani. Huenda kuna matatizo kwa upande wa wanafunzi ambao wanatamauka au kwa upande wa usimamizi wa kazi za wanafunzi ambapo wasimamizi hawana muda wa kutosha kusoma kazi za wanafunzi.

**Jedwali 1: Idadi ya wanafunzi waliofuzu kila mwaka katika kiwango cha uzamili**

| Mwaka wa kufuzu | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|
| 1990 | 4 |
| 1991 | 6 |
| 1992 | 3 |
| 1993 | - |
| 1994 | 3 |
| 1995 | - |
| 1996 | 3 |
| 1997 | 2 |
| 1998 | - |
| 1999 | - |
| 2000 | - |
| 2001 | 3 |
| 2002 | 3 |
| 2003 | 3 |
| 2004 | 3 |
| 2005 | 16 |
| 2006 | 5 |
| 2007 | 13 |
| 2008 | 15 |
| 2009 | 7 |
| 2010 | 5 |
| 2011 | 15 |
| 2012 | 14 |
| 2013 | 8 |
| 2014 | 18 |
| 2015 | 16 |
| **Jumla** | **165** |

Katika miaka ya 2005 na kuenda mbele tunaona idadi ya wanafunzi wanaofuzu ikiongezaka. Hali hii inatokana na vyuo vikuu kufungua milango kwa wanafunzi ambao walikuwa wamehitimu katika daraja ya Diploma ili waweze kuendeleza

masomo yao katika kiwango cha shahada ya kwanza. Baadaye, wanafunzi hawa waliendelea na masomo ya uzamili. Kikazi, wanafunzi wamepata motisha kutokana na wengi wao kupandishwa madaraka baada ya kupata shahada ya kwanza na hata ya uzamili. Vilevile, kuanzishwa kwa masomo maalumu ya walimu vyuoni, ambapo walimu wanaweza kujiendeleza kimasomo nyakati za likizo za shule, hasa Aprili, Agosti na Desemba kumewawezesha wanafunzi wengi kujisajilisha katika programu ya uzamili. Sababu nyingine inatokana na sekta ya benki kulegeza utoaji wa mikopo kwa wanajamii. Hali hii imewawezesha walimu kuchukua mikopo ya kugharamia masomo yao.

**Jedwali 2:Idadi ya wanafunzi waliofuzu katika kiwango cha uzamifu**

| | |
|---|---|
| 1998 | 3 |
| 2003 | 1 |
| 2004 | 1 |
| 2006 | 1 |
| 2008 | 2 |
| 2012 | 1 |
| 2014 | 2 |
| 2015 | 3 |
| **Jumla** | **14** |

Inavyobainika kutokana na jedwali (2) hili ni kwamba, idadi ya wanafunzi wanaojiunga na programu ya uzamifu ni wachache mno. Kama tulivyoeleza hapo awali, suala la kugharamia masomo limekuwa changamoto kwa wanafunzi wengi. Vilevile, muda wanaochukua wanafunzi kukamilisha masomo ya uzamifu linaweza kuwa jambo linalowavunja moyo wanafunzi wengi walio na nia ya kujiunga na programu ya uzamifu.

**Vitengo Maalumu katika Fasihi**

Katika kuangazia vitengo maalum, idara hufunza masomo ya fasihi na isimu na tumeonyesha idadi ya tafiti ambazo zimefanywa katika maeneo haya (taz Jedwali 1&2). Uga wa fasihi umegawika katika matawi matatu ambayo ni fasihi andishi, fasihi simulizi na fasihi ya watoto. Kwa mujibu wa mitaala ya vyuo vikuu nchini, masomo ya kijumla yanayoshughulikiwa ni pamoja na historia ya fasihi, nadharia za uhakiki, fasihi simulizi, fasihi ya watoto fasihi ya kisasa, fasihi - linganuzi na uchambuzi wa maandishi.

Uhakiki katika fasihi ya Kiswahili unaonekana kupiga hatua hasa katika fasihi andishi na fasihi simulizi. Hatua hizi zinatokana na shughuli za awali kama vile utafiti

uliopelekea kuchapishwa kwa makala ya kitaaluma katika majarida mbalimbali na uchapishaji wa vitabu vilivyodhamiriwa kutumiwa katika somo la uhakiki katika vyuo vikuu, (Mbatia, 2002; Mbaabu, 2005). Ukweli ni kwamba pamekuwa na mchango mkubwa kutoka katika Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili- TATAKI (iliyokuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili – TUKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika nyanja tofauti za maendeleo ya Kiswahili. Hatua hii iliweka misingi ya kuchunguzia lugha na fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, kuanzia nusu ya pili ya muongo wa 1970 na nusu ya kwanza ya muongo wa 1980, TUKI ilipiga hatua ya kuunda msamiati wa kutosha wa kuandika vitabu vya masomo mbalimbali katika shule za sekondari kwa Kiswahili. Vilevile, utangaji upya wa kamusi, uundaji wa istilahi na tafsiri ni shughuli ambazo zingali zinaendelea na ambazo zimechangia makubwa katika uelewa wa dhana mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili. Katika eneo la fasihi andishi tunapata takribani tafiti 65, na katika kitengo cha fasihi simulizi tunapata kuwa tafiti 24 zimefanywa. Tafiti zilizoshughulikiwa katika fasihi ya watoto ni 9.

**Jedwali 3:Maeneo katika fasihi katika kiwango cha uzamili**

| | |
|---|---|
| Fasihi andishi | 65 |
| Fasihi simulizi | 24 |
| Fasihi ya watoto | 9 |
| **Jumla** | **98** |

**Jedwali 4: Maeneo katika fasihi katika kiwango cha uzamifu**

| | |
|---|---|
| Fasihi andishi | 4 |
| Fasihi simulizi | 4 |
| Fasihi ya watoto | - |
| **Jumla** | **8** |

Fasihi andishi inaonekana kushughulikiwa kwa kiwango kikubwa katika kiwango cha uzamili. Hii huwa njia ya rahisi kwa sababu haimgharimu mtafiti hela nyingi. Katika eneo hili, mwanafunzi hahitaji kwenda nyanjani kufanya utafiti kama ilivyo katika eneo la fasihi simulizi bali huufanyia maktabani. Fasihi simulizi huwa na gharama kwa mtafiti na huweza kuchukuwa muda mrefu. Pia, kuna ukosefu wa vifaa maalumu vya nyanjani, hivyo basi, wanafunzi wengi hujiepusha na eneo hili.

Katika eneo la fasihi ya watoto, tunaona kuwa ingawa kozi hii imekuwa ikifunzwa katika idara hii tangu mwaka wa 1997, katika kiwango cha shahada ya kwanza, ni kufikia tu mwaka wa 2002 ambapo tunaona kuwa eneo hili limeanza kufundishwa katika kiwango cha uzamili na sasa baadhi ya wanafunzi wamejitosa katika uga huu na kuufanyia utafiti (Ngugi, 2012 & 2014). Huenda motisha ya kufanya utafiti katika eneo hili linatokana na asasi mbalimbali kuanza kuchangamkia fasihi ya watoto.

Kwa mfano, tunaona kuwa, kuanzia mwaka wa 2003 ambapo Taasisi ya Utungaji Mitaala - Kenya ( iliyokuwa Taasisi ya Elimu) ilipobadilisha silabasi ya Kiswahili na kujumuisha somo la fasihi, palikuwa na uchapishaji mwingi wa vitabu vya watoto. Vilevile, mashirika ya uchapishaji yamechangia pakubwa katika kupatikana kwa fasihi ya watoto kutokana na kuchapisha vitabu vingi vya watoto. Pia serikali imegharamia pakubwa ununuzi wa vitabu vya watoto katika shule nyingi za serikali ( Ngugi, 2014). Hali nyingine inatokana na sababu kuwa, kozi hii hufundishwa katika digrii ya kwanza tofauti na ilivyo katika vyuo vingine, hivyo basi wanafunzi huwa wamepata msingi imara wa kuendelea na kozi hii wanapojiunga na programu ya uzamili.

Katika kuchunguza tanzu zilizoshughulikiwa katika fasihi andishi ya watu wazima, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali 5: Tanzu zilizoshughulikiwa katika fasihi Andishi**

| | |
|---|---|
| Riwaya | 27 |
| Tamthilia | 14 |
| Ushairi | 20 |
| Hadithi Fupi | 4 |
| **Jumla** | **65** |

Utafiti huu unadhihirisha maoni ya Mohochi (2002) kuwa, licha ya kuwa na historia ndefu na kutekeleza majukumu muhimu katika jamii, kwanza katika masimulizi na kama hadithi ya kubuni, hadithi fupi haijashughulikiwa wala kuendelezwa katika viwango sawa na tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili. Pengine malighafi katika eneo hili yalikuwa haba mno hadi kufikia miaka ya 2002 ambapo utanzu huu uliweza kutambuliwa na kufundishwa katika viwango mbalimbali vya elimu kuanzia shule za upili hadi vyuo vikuu. Hata hivyo, matokeo yanadhihirisha kuwa utanzu huu ungali unafanyiwa uchunguzi mchache. Katika utanzu wa fasihi simulizi, eneo liliofanyiwa utafiti kwa wingi ni eneo la nyimbo, lifuatwa na methali. Tunaweza kuchukulia kuwa wanafunzi wengi wanapata malighafi za kutosha wanapofanya utafiti katika kipera cha nyimbo. Tazama jedwali la 6 hapa chini.

**Jedwali la 6: Tanzu zilizoshughulikiwa katika fasihi simulizi**

| | |
|---|---|
| Nyimbo | 14 |
| Methali | 4 |
| Vichekesho | 2 |
| Vitendawili | 2 |
| Utendi | 2 |
| **Jumla** | **24** |

Uchunguzi zaidi kuhusiana na tafiti hizi umeonyesha kuwa katika kazi hizi zote, nadharia mbalimbali zimetumikizwa. Kwa mujibu wa Indede (2002) nadharia hutumiwa katika kuelewa na kuongoza masuala ya utafiti. Vilevile, nadharia husaidia katika kuunda mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data pamoja na kutumiwa kwa minajili ya kupata fahiwa kutokana na mifumo mbalimbali ya data iliyokusanywa. Kwa kuzingatia umuhimu huu wa nadharia, inabainika kuwa, kuna watafiti walioshughulikia nadharia mbalimbali za kimtindo, mwingilianomatini, diskosi za usemi na nyingine nyingi ili kuongoza utafiti wao. Wengine wametumia nadharia ya mtazamo-kike, nadharia ya kiuhalisia wa kijamii, nadharia ya kiuhalisiaajbu, nadharia ya ujumi mweusi na nadharia ya Unisai na urasimu miongoni mwa nadharia nyinginezo. Kwa hakika, wanafunzi hawa wametambua nadharia mpya ambazo zinaibuka na kuzijaribia masuala ya utafiti wao. Hii ni hatua nzuri katika maendeleo ya utafiti wa Kiswahili ikilinganishwa na ilivyo kuwa miaka ya zamani ambapo wanafunzi wengi waliegemea kwenye nadharia ya U- Marx na uyakinifu wa kijamii kama ilivyo bainika na Musau na Ngugi, (1997). Mwegemeo huu ulitokana na hali ya uandishi ya wakati huo ambapo waandishi mbalimbali walishughulikia masuala ya ukoloni kwa wingi ( Khamis, 2002). Kama anavyodai Khamis, (Keshatajwa), waandishi wa hivi sasa hasa kuanzia miaka ya 1980, wanafanya majaribio mengi katika uandishi huku wakiibuka na mbinu anuwai za kuandika kazi zao, jambo ambalo limechochea uzinduzi wa nadharia mpya za kuchanganulia kazi hizi. Vilevile, utumikizi wa nadharia mbalimbali yanatokana na mafunzo ya kinadharia wanayopata wanafunzi hawa katika kozi zao za awali na hata katika kiwango cha uzamili.

**Vitengo Maalumu katika Isimu**

Uwanja wa isimu ni mpana na hujumuisha matawi kama vile, Isimu-historia, isimu-linganishi, isimu-falsafa, isimu-muundo na isimujamii miongoni mwa matawi mengine. Katika utafiti huu, ilibainika kuwa jumla ya tafiti 67 zimeshughulikia maeneo mbalimbali ya isimu katika kiwango cha uzamili na 6 katika kiwango cha uzamifu.

**Jedwali la 7:Maeneo yaliyoshughulikiwa katika isimu**

| | |
|---|---|
| Fonetiki | 1 |
| Fonolojia | 11 |
| Mofolojia | 2 |
| Mofosintaksia | 4 |
| Sintaksia | 8 |
| Ujifunzaji wa lugha ya pili | 4 |
| Leksia | 5 |
| Isimujamii | 21 |
| Isimu amali | 4 |
| Tafsiri | 5 |
| Teknolojia na mawasiliano | 2 |
| **Jumla** | **67** |

Idadi kubwa ya tafiti inaonyesha kuwa, wanafunzi wamezama katika kuangalia masuala ya kiisimujamii hasa mielekeo ya wanajamii kuhusu masuala mbalimbali ya lugha. Nadharia mbalimbali zimeshughulikiwa pia katika eneo hili, zikiwemo, Nadharia za kifikra na kivitendo, nadharia ya uchanganuzi makosa, nadharia ya uzalishaji, nadharia ya umuundo miongoni mwa nadharia nyinginezo. Ingawa eneo hili halijashughulikiwa kwa wingi, hali ilivyo ni kwamba maeneo mbalimbali yameweza kutafitiwa ikilinganishwa na ilivyo kuwa hapo zamani (Taz. Musau na Ngugi, 1997). Ongezeko hili linatokana na upatikanaji wa vitabu vya isimu ambavyo vinachapishwa hivi karibuni. Hata hivyo, tatizo kubwa linatokana na ugumu wa kuelewa nadharia ambazo nyingi zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na hulazimu wanafunzi kuzitafsiri na kuzitumia katika tafiti zao.

**Changamoto**

Zipo changamoto kadhaa ambazo idara hii inakumbana nazo; mojawapo ya changamoto hizi inatokana na idadi ya wasimamizi dhidi ya idadi ya wanafunzi waliojisajili idarani. Hivi sasa, mwalimu mmoja anasimamia takribani wanafunzi arobaini hasa katika eneo la fasihi. Hali ambayo ni kinyume na matakwa ya Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu. Hii ina maana kuwa wanafunzi wengi wemejisajili katika kiwango cha uzamili. Kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na chuo hiki na kujiunga na idara ya Kiswahili, wahadhiri wengi wanajipata wakiwa wametwika mzigo mzito wa kufundisha na hata kuwasimamia wanafunzi wa uzamifu katika utafiti wao. Pili, wanafunzi wengi wanachukua muda mrefu kukamilisha kazi zao kutokana na sababu kuwa hata wao wanayo majukumu mengine kama walimu wa shule za msingi au sekondari. Hivyo basi, idadi ya wanaojiunga na programu hii haiambatani na ile ya wanaokamilisha.

## Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa ni kuchunguza hatua za kimaendeleo katika tafiti zilizofanywa katika idara ya Kiswahili ya Chup Kikuu cha Kenyatta. Inaelekea kuwa tafiti nyingi zimeweza kufanywa katika fasihi kuliko ilivyo katika isimu. Hii ina maana kuwa mwelekeo wa wanafunzi katika idara hii imekuwa ni kushugulikia masuala ambayo wanaona kuwa wanaweza kujitambulisha nayo moja kwa moja kijamii. Hata hivyo, eneo la isimu limeanza kutambuliwa na wanafunzi wengine. Hii ni kutokana na hali kuwa, kwa sasa kuna makala na vitabu ambavyo vinashughulikia eneo hili kwa Kiswahili, kwa hivyo machapisho haya yanaendeleza uelewa wa somo hili.

## Marejeleo

Indede, F.N. (2002). Masuala ya Nadharia na Taratibu katika Utafiti wa Tasnifu za Kiswahili. Katika : Inyani Simala (Mh.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press. 22-24.

Khamis, S. A.M. (2002). Defamiliarization, Expeimentation and the Future of Swahili Literature. Katika : Inyani Simala (Mh.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.190- 213.

Mbaabu, I. (2005).Mchango wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) katika Unedelezaji na Ukuzaji wa Kiswahili. Katika *Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Jarida Maalumu la TUKI. 84 – 93.*

Mbatia, M. (2002). Hatua za Maendeleo ya Uhakiki wa Fasihi nchini Kenya. Katika: Inyani Simala (Mh.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.149-154.

Ministry of Education. (2002). *Ministry of Education and Technology: Primary School Education Syllabus*. Volume 1. Nairobi: Ministry of Education.

Ministry of Education. (2007). *Approved List of Primary and Secondary Schools Textbooks and other Instructional Materials*. Nairobi: Ministry of Education.

Mohochi, E.S. (2001). "Fasihi ya Kiswahili katika karne ya 21: Nafasi ya hadithi fupi." Katika: J.S. Mdee & H.J.M. Mwansoko, *Makala ya Kongamano la Kimataifa. Kiswahili 2000*. TUKI. 62-74

Musau, P. & Ngugi, P.M. Y (1997). Kiswahili Research in Kenyan Universities: Where are we Now? Katika *Swahili Forum* AAP 51.219-229 .

Ngugi, P.M.(2012). Mitaala ya Kiswahili katika Elimu na Utaifa: Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Uendelezaji na Uimarishaji wa Utaifa. Katika: Clara Momanyi na Wengine (Wah). *Kiswahili na Utaifa*. Nairobi: Twaweza Communications na CHAKITA. 106-120

Ngugi, P. (2014). Miaka Hamsini ya Fasihi ya watoto katika Kiswahili nchini Kenya: Maendeleo na Changamoto. Katika: I. Simala na wengine (Wah).*Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications na CHAKITA. 16-33.

Republic of Kenya. (1964). Report of the National Committee on Educational Objectives and Policies. Nairobi: Government Printers.

Simala, I. (2002). Miradi ya Utafiti katika Vyuo Vikuu mnamo karne ya Ishirini na moja. Katika: Inyani Simala (Mh.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret, Moi University Press.11-21